Mimi Ndimi Ufufuo Na Uzima

. . .Siwataki ninyi. . .msijue, ndugu, habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.

Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao. . .waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.

Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti.

Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko,. . .sauti ya malaika mkuu, na. . .parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.

Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao. . .katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani;. . . na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.

Basi farijianeni kwa maneno hayo.

2 Nilikuwa ninasoma kutoka katika Wathesalonike wa Kwanza, mlango wa 4. Nitasoma sasa kutoka katika Kitabu cha Ayubu. Ninii ya nne-. . .Mlango wa 14 wa Ayubu.

Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke, siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu.

Yeye huchanua kama vile ua, kisha hukatwa; hukimbia kama kivuli, wala hakai kamwe.

. . .je! wafumbua macho yako kumwangalia mtu kama yeye, na kunitia katika hukumu pamoja nawe?

Ni nani awezaye kutoa kitu kilicho safi kitoke katika kitu kichafu? Hapana awezaye.

Kwa kuwa siku zake zimeamriwa, hesabu ya miezi yake unayo wewe, nawe umemwekea mipaka yake asiyoweza kupita;

Acha kumwangalia yeye, apate kupumzika, hata atakapotimiza siku *zake, kama aliyeajiriwa.*

Kwani yako matumaini ya mti, ya kuwa ukikatwa,. . . utachipuka tena, wala machipukizi *yake hayatakoma.*

Ijapokuwa mizizi yake huchakaa mchangani, na shina lake kufa *katika udongo;*

Lakini kwa harufu ya maji utachipuka, na kutoa matawi kama mche.

Lakini mwanadamu hufa,. . .huifariki dunia; naam, mwanadamu hutoa roho, naye yupo wapi?

Kama vile maji kupwa katika bahari, *na* gharika kupunguka *na* kukauka*;*

Ni vivyo mwanadamu hulala chini, asiinuke*; hata . . . wakati wa mbingu kutokuwako tena, hawataamka, wala kuamshwa usingizini.*

Laiti ungenificha kuzimuni, ukanilinda *kwa siri,* hata *ghadhabu zako zitakapopita,. . .na kuniandikia . . . muda ulioamriwa, na kunikumbuka!*

Mtu akifa*, je! atakuwa hai tena? Mimi ningengoja siku zote za muda wangu ulioamriwa, hata kufunguliwa kwangu* kunifikilie.

Wewe ungeita,. . .nami ningekujibu; Ungekuwa na tamaa ya kazi ya mkono *wako.*

. . .sasa wazihesabu hatua zangu; je! huchungulii dhambi *zangu?*

Makosa yangu yametiwa muhuri mfukoni,. . .nawe waufunga uovu wangu.

. . .kwa kweli milima ikianguka *hutoweka,. . .nayo* majabali huondolewa *mahali* pake*;*

Maji mengi huyapunguza mawe; wewe waondolea mbali vitu vimeavyo kutoka kwa mavumbi ya nchi; nawe huangamiza matumaini ya mwanadamu.

Wewe wamshinda nguvu sikuzote, naye hupita *aende zake;* wabadili sura *zake, na* kumpeleka *aondoke.*

Wanawe wafikilia heshima, wala . . .yeye hajui;. . . kisha wao huaibishwa, lakini . . .yeye hana habari . . .

Lakini mwili ulio juu yake una maumivu, na nafsi yake ndani huomboleza.

3 . . .-moja na mlango wa 14 wa Kitabu cha Ayubu.

4 Tunacho hapa, alasiri ya leo, kitu ambacho hakitakiwi mahali popote wakati wowote. Haijalishi jinsi tulivyojiandaa kwa ajili yake, kila mara ni mgeni asiyekaribishwa aliye na hakika kuja katika kila boma. Na hakina huruma. Nina hakika kama ningalikuwa ni kifo, sidhani ningetaka kuja katika boma ambalo kifo hiki kimekuja, huyu Mkristo mchanga, ambaye tuna mwili wake umelazwa hapa mbele zetu, kama tunavyomfahamu, kama Ndugu yetu Garnett.

5 Basi tupo hapa leo hii, tumekusanyika, kutoa heshima za mwisho kwa kijana huyu, Mkristo hodari. Ndiyo mambo ya mwisho tunayoweza kumfanyia juu ya nchi, ingawa yeye hatusikii. Lakini tunawaza kuhusu wale walio na hiki mbele zao, bado. Hakina budi kushughulikiwa siku moja. Hatuna budi kukabiliana nacho. Vijana au wazee, hapana budi, kitatujia sote.

6 Haijalishi kile ningeweza kusema kuhusu Garnett, kama nilivyomjua, hakitabadilisha maoni yetu. Maisha yake na ushuhuda wake unanena, miongoni mwenu nyote, kwa sauti kubwa kuliko chochote ningaliweza kusema. Mimi . . .

7 Kujuana kwangu na yeye kulikuwa ni kupitia kwa mama yake. Usiku mmoja, ibada ilipokuwa imekamilika, kwenye . . . kanisa langu, alinijia. Na yeye alikuwa na mwana aliyekuwa anakufa kwa polio. Nafikiri walikuwa wamepoteza matumaini kwamba angeweza kuishi zaidi. Vema, nyingi ya ziara hizo, tunazo. Ni desturi tu za kawaida. Lakini nilipoenda kumwona kijana huyu, alikuwa kwenye mashine ya kuvutia hewa. Kulikuwa na kitu kumhusu, vile nilivyomwona kwa mara ya kwanza, nilimpenda. Ninampenda hata leo, ninapomtazama sasa, daima nitampenda. Alikuwa ni kijana hodari. Na ilionekana kama alikuwa na kitu maishani ambacho—ambacho kilimaanisha zaidi ya mvulana tu wa kawaida, wa tineja anayepitia tu. Alikuwa na ufahamu mzuri zaidi wa mambo. Nilimwombea, kwamba asife.

8 Hatimaye, walimtoa kwenye mashine ya kuvutia hewa, naye akaletwa nyumbani, akawekwa katika namna ya kitanda cha kupembeza, ambapo wanamweka kupumua.

9 Nilikuja kumwona Garnett. Na jinsi ambavyo maisha hayo yalikuwa yamekua kuwa Mkristo mwema, mvulana ambaye—ambaye mzazi yeyote angejivunia. Hata hivyo, hiyo ni ninii yetu—hiyo ni safari yetu hapa duniani, hiyo ndiyo sababu yake, ni kujiandaa kwa ajili—kwa ajili ya kuondoka. Naye Garnett kwa hakika alikuwa amefanya maandalizi haya, kupita kivuli chochote cha shaka, kijana hodari aliyejaa Roho na Uzima wa Kristo. Ilijiakisi moja kwa moja kupitia yeye.

10 Nami ninaishi Tucson, Arizona. Wakati fulani uliopita, mvulana huyo mdogo alikuwa mgonjwa, na alikuwa mgonjwa sana. Na dhihirisho la imani yake, kupiga simu mwendo mrefu. Basi wakati hatimaye nilifika nyumbani kwangu na kumwombea mvulana huyo mdogo, kwenye simu, mbona, neema ya Mungu ilimjia, na a—akapona. Muda baada ya muda, wakati tungekuwa na kitu kasoro, a—angepiga simu. Pamoja tungeomba, kwa njia ya simu. Nami sidhani Baba yetu wa Mbinguni aliwahi kumkataa, wakati wowote, ila kwamba alishinda kile alichokuwa nacho.

11 Majira ya kupukutika yaliyopita, nilikuwa huku chini nikiwatembelea marafiki. Siku moja, mara ya mwisho niliyomwona Garnett katika maisha haya, tuliingia bila kutarajiwa kwenye . . . nyumba yake ndogo ya kupendeza. Alikuwa anakaa na watu wake. Basi tulikuta nini, bali ingekuwa ni m—mfano halisi kwa Mkristo yeyote mhudumu ku—kuona hili. Alikuwa anaamka, na kutoka kwenye kitanda cha kupembeza, alikuwa na mikono yake katika kitambaa cha

kuchukulia mkono. Na tulipotembea kuenda nyumbani, kwa kuwa daima tulikuwa tumekaribishwa sana, huyo hapo alikuwa Garnett. Na mbele yake kulikuwako Biblia. Na maskini mama aliyekuwa akimhudumia alikuwa ameketi juu ya maskini kitu kilichokunjwa mara mbili, nao walikuwa wanafanya somo la Biblia. Ndipo nikamwangalia, na moyo wangu ukayeyuka tu.

12 Ndipo nikamwambia, nikamwuliza swali. Nikasema, "Garnett, labda, vipi kama jambo hili halikuwa limekutokea?" Tena nikasema, "Ungeninii. . .niliitwa, tuseme, hapa juu usiku wa leo, kulikuwako na mvulana mdogo jina lake Garnett Peake alikuwa ndiyo kwanza auawe hapa nje barabarani, na motokaa yake. Na mvulana huyo alikuwa amelewa, na nafsi yake ilikuwa imeenda kukutana na Mungu. Ama, je! ungetaka kuacha mandhari jinsi ilivyo?"

13 Akasema, "Acha tu iwe jinsi ilivyo. Mradi tu ninamjua Yesu jinsi ninavyomjua sasa," akasema, "ni zaidi ya uhai, hata ingawa ingenibidi kukaa hapa maisha yangu yote katika hali hii."

14 Lakini yeye akasema, "Ninataka kukuonyesha, Ndugu Branham, niko afadhali zaidi." Angeweza kusogeza mikono yake, na kadhalika. Kwa matarajio makubwa, alikuwa anatazamia wakati ambapo angekuwa mzima, ili aweze kutembea kote. Mimi ni mzee, nimeona mengi katika siku zangu. Sidhani nimewahi kukutana na mvulana mwenye roho shujaa zaidi ya Garnett. Matumaini makubwa kwake.

15 Siku chache zilizopita usiku, ninaambiwa kwamba alichukua. . .alishikwa na kitu kama homa ya matumbo. Na kwamba wakati alipotambua kwamba alikuwa yuaenda, vema, aliniita. Naye hakujua, wakati huo, nilikuwa New York, kwenye uwanja. Basi nilipotoka kwenye uwanja, telegramu, ama ujumbe ulitolewa kwangu. Niliharakisha upesi kwenye simu na kupiga simu. Lakini ndugu mpendwa anayemtunza, kasema, "Ndugu Branham, Garnett alienda kukutana na Yesu, saa kumi na mbili."

16 Ametuacha. Tu—tunatambua hilo. Ila sijui kama kweli kuna jambo kama—kama huu kuwa ndio mwisho wake? Sote tunafahamu kwamba mvulana huyo ametuacha, ni maisha, lakini hebu tuwazie kinachofuata. Je! kuna jambo lolote tunaloweza kusema, hivi tunaweza kumwona tena? Je! hii ndiyo mara ya mwisho tutakapomwona Garnett? Hilo ndilo ninalotaka kuwazungumzia juu yake, kwa dakika chache zijazo. Je! unaweza kuwa na hakika kwamba tunaenda kumwona tena? Ayubu aliuliza swali hili, Kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia. Akasema, "Mwanadamu akifa, je! ataishi tena?" Je! kuna thibitisho lolote basi kwamba hivi ndivyo ilivyo? Je! tunaweza kuwa na thibitisho lolote la kimwili kwamba ufufuo huu ni hivyo? Naam. Naweza kuwazia hivyo.

17 Kama tukitambua, kwamba, tunamtumikia Muumba. Tunatambua kwamba hatungeweza kuwa hapa isipokuwa kuwe na kitu fulani ambacho kilitufanya. Hatuwezi tu kuwa jinsi tulivyo, bila ya ku—kutokea tu kuwa; si zaidi ya vile saa yangu ingeweza tu kuwa jinsi ilivyo, pamoja na vito vyote na utunzaji saa. Kulikuwa na. . . Kuna akili anzilishi nyuma yake, iliyotengeneza hiyo saa, na hebu wazia tu kile alicho mwanadamu anayeitengeneza hiyo saa. Jinsi ambavyo isingewezekana kwa hiyo saa kutokea tu, na jinsi isivyowezekana zaidi kwamba sisi tulitokea tu!

18 Kwa kuwa mmishenari na kusafiri kote ulimwenguni, nimezoea sasa, mara saba kuuzunguka ulimwengu, na kuwazia kuona dini mbalimbali za ulimwenguni, na kila moja ya falsafa zao na kile wanachowazia. Na wengi wao wana imani kuwa roho ya marehemu huingia katika mwili mwingine, na kadhalika. Lakini dini ya Kikristo ndiyo dini ya pekee iliyo na kweli, kwa sababu maumbile yote yananena kuhusu Ukristo.

19 Ayubu alisema, "Mti ukifa, kuna matumaini kwamba u—utaishi tena. Na ua likifa, kuna matumaini kwamba litaishi tena." Bali akasema, "Mwanadamu hulala chini, naye hutoa roho, naye yuko wapi?" Ayubu alikuwa ni mwanadamu, m—mtu aliyejulikana. Alikuwa ni m—mwanafalsafa mashuhuri wa siku yake, na mwaminio, na alikuwa na hekima nyingi. Basi Shetani alitamani ku—kumpepeta na kumjaribu.

20 Na Wakristo wote, waaminio, wanajaribiwa. "Kila mwana amjiaye Mungu lazima ajaribiwe, acharazwe."

21 Kwa hiyo, Ayubu, akijua kwamba Muumba aliumba viumbe Vyake vyote, alitambua kwamba katika maumbile, kwamba, kulikuwa na ufufuo wa uhai wa mimea, kadhalika. Bali akasema, "Mwanadamu hulala chini, yeye hutoa roho, anaaga dunia, naye yupo wapi? Ni kitu gani kilichomfanyikia?"

22 Ndipo basi akaona, kwa ono, kuja kwa Yule Mwenye haki. A—alijua alikuwa ni mwenye dhambi. Na sa—sababu ilimbidi mwanadamu kulala chini, asiinuke, hakukuwa na kitu kingaliweza kumtetea.

23 Alijua kwamba ua halikuwa limefanya chochote. Lililetwa hapa kwa kusudi, nalo likatumikia kusudi la Mungu. Na, hivyo basi, ua lilipokufa, lingeweza kufufuka tena.

24 Lakini mwanadamu alikuwa ametenda dhambi, na hakukuwa na njia kwake kuwahi kusimama katika Uwepo wa Muumba wake. Na kwa hiyo, katika hali hii, aliruhusiwa na Mungu kumwona Yule Mwenye haki akija. Mtu Ambaye angeweza kuweka mikono Yake juu ya mwanadamu mwenye dhambi na Mungu mtakatifu, na kuunganisha njia, Mwana wa Mungu. Ndipo wakati Roho alipokuwa juu ya nabii, alilia kwa sauti, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi, na ingawa baada ya

mabuu ya ngozi yangu kuuharibu mwili wangu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu mimi mwenyewe. Macho yangu yatamwona, na si mwingine."

25 Ukristo wote umetiwa msingi juu ya ufufuo. Hayo ndiyo matumaini yetu. Sasa hebu tuone ni kwa nini. Muumba ameyaweka katika utaratibu sana, kama hatukuwa hata na Biblia, bado tungeweza kujua kwamba Ukristo ulikuwa sahihi.

26 Sasa, ufufuo si kuweka kitu badala ya kingine. Ufufuo ni kuinua kitu kile kile kilichoingia chini. Kama nikiangusha Biblia kutoka kwenye—kwenye kiweko, kianguke sakafuni, na kushika ninii, Biblia nyingine, na kuiweka badala yake, huko ni kuweka kitu badala ya kingine. Lakini, ufufuo, ni kuileta Biblia ile ile iliyoanguka. Na hiyo ndiyo *ufufuo* unayomaanisha, "ku—kufufuliwa."

27 Na, Mungu, Muumba mkuu Ambaye amejidhihirisha Mwenyewe kupitia maumbile Yake yote. Na sisi ni sehemu ya maumbile Yake, kama tu vile maua hayo yalivyo, kama tu vile miti ilivyo, maumbile yote mengine. Sisi ni sehemu ya maumbile Yake.

28 Sasa, Mungu ni Mungu wa vitu vya namna mbalimbali. Hana kila kitu cha aina ile ile. Hana vitu vyote kuwa ni milima tu. Ana jangwa, sehemu tambarare, makonde ya nyasi. Pia ana maua ya manjano, meupe, samawati, yenye rangi ya waridi, rangi tofauti tofauti. Yeye ana watu wanene, watu wadogo; na wenye kichwa cheusi, wenye kichwa cha hudhurungi, kichwa chekundu. Yeye ni Mungu wa vitu aina mbalimbali, kwani kila kitu kinafaa kutumikia kusudi Lake. Anacho kila kitu kutumikia kusudi Lake. Na kila kitu kinachotumikia kusudi Lake, kwa njia sahihi, kuna kufufuka kwake.

29 Sasa, hilo huenda likawa gumu kuwazia au kuelewa, mara moja, bali hebu tuliwazie, kwa kuwa tunalo hili hapa mbele zetu, alasiri hii.

30 Sasa, haya hapa maua. Yanadhihirisha kile kilichoyaleta hapa duniani, kusaidia kuchangamsha chu—chumba chenye uchovu, alasiri ya leo, ambapo huyu ndugu kijana mpendwa amelala, usingizi. Na hayo maua, tunatambua.

31 Kama nyinyi wanawake hapa Kentucky. Ni—ninatoka hapa, mimi mwenyewe. Na—na ninatambua mnapanda maua yenu kuzunguka nyumba yenu, na—na majira ya joto yananawiri vizuri sana, na kuangaza nyumba yenu. Halafu basi, labda, majira ya kupukutika ya mwaka, ghafla, jalidi huyapiga. Hicho ni kifo. Sasa, kama tayari petali zinaanguka, au kama ni maua machanga, au chochote yalicho, jalidi ikipiga, huyachukua yote. Hicho ni kifo. Hakipendelei mtu, uwezo, umri. Kinapiga tu. Na mahali kinapopiga, kinachukua. Halafu tunaona petali zinaanguka kutoka kwa maskini ua hilo, basi, na kutoka kwenye ua huanguka mbegu ndogo nyeusi.

32 Na sasa huenda hii ikaonekana ya kitoto. Lakini hivyo ndivyo unavyompata Mungu, ni katika vitu rahisi, si vi—vitu vyenye utata. Mungu amelifanya rahisi, kama tu tungeweza kuliona.

33 Sasa, Mungu anao msafara wa mazishi kwa ajili ya ua hilo; inaonekana ya kigeni. Bali mbegu hiyo ndogo imekaa ardhini. Halafu mvua ya mapukutiko inakuja, kama machozi yakidondoka kutoka angani, na kupigapiga juu ya maskini mbegu hii, mpaka inaizika.

34 Kisha moja kwa moja kunakuja majira ya baridi kali. Sasa, petali zimekwisha. Shina limekwisha. Kitunguu ardhini, mizizi imekauka. Loo! Mbegu, majira ya baridi yakiganda, hugandisha mbegu. Hupasua na kuifungua mbegu, nyama hutoweka. Sasa tunaelekea, Februari au Machi. Hakuna petali, hakuna shina, hakuna mbegu, hakuna nyama ya mbegu, hakuna chochote.

35 Je! huo ndio mwisho wa ua hilo? Si hata kidogo. Kuna chembe ndogo ya uhai, mahali fulani, ndani ya mbegu hiyo. Hiyo, unaweza kuchukua udongo mikononi mwako, na kuupeleka kwenye maabara, na kumfanya m—m—mwanasayansi auchunguze, huku na huko, naye kamwe hataipata hiyo chembe ya uhai. Mungu aliificha. Lakini punde tu u—ulimwengu unapozunguka katika mfumo wa jua, mpaka una...mpaka unazunguka kufikia mahali jua linaanza kuipiga dunia tena. Usingeweza kuuficha uhai huo.

36 Kama ulitengeneza kijia cha saruji, kupitia uani mwako, juu ya nyasi, iko wapi ninii yako inayofuata...ninii zaidi...Majira ya joto yanayofuata, nyasi nyingi ziko wapi? Moja kwa moja kandokando ya kijia. Kwa nini? Ni ule uhai uliokuwa umelala chini ya hiyo—hiyo saruji. Na inapofika majira ya kuchipua, ingawa jiwe liko juu yake, halitauficha. Uhai huo utapenyeza njia yake moja kwa moja. Hiyo ndiyo inayofanya nyasi nyingi sana karibu na ukingo wa hicho kijia. Huwezi kuficha uhai. Hauna budi kuchipuka kwa sababu Mungu ameweka jua, j-u-a, juu ya huu, uhai wa mimea, nalo hutawala uhai wa mimea.

37 Vema, kama Yeye aliweka j-u-a juu ya uhai wa mimea, basi aliweka M-w-a-n-a Wake juu ya Uzima wa Milele. Kwa hiyo, ikiwa kuna ufufuo wa ua, kwa sababu lilitumikia kusudi la Mungu, ni zaidi jinsi gani Yeye alivyofanya njia kwa mwanadamu! Naam. Ipo njia kwa mwanadamu. Hana budi kufufuka, pia, ukiwadia wakati kwa ajili ya M-w-a-n-a wa Mungu. Si...J-u-a, huleta uhai wa mimea, kwa sababu hutawala huo. Huwezi kuuficha. Hauna budi kuchipuka. Pia yupo M-w-a-n-a wa Mungu anayetawala uhai wa wanadamu, Uzima wa Milele. Na kama tunatumikia kusudi la Mungu, kama wana na binti za Mungu, basi wakati utakapokuwa tayari kwa M-w-a-n-a wa Mungu kuja, usingeweza kuuficha Uhai huo. Maumbile yote yanazungumzia Huo.

38 Tuko hapa katika majira ya kupukutika ya mwaka huu, hapa Kentucky, ambapo miti ya kupendeza ambayo mwaka huu imechipuza majani yao. Halafu basi, kabla hata hatujawa na ja—jalidi yoyote au chochote, Hivi mlitambua katika nyua zenu na kote, jinsi ambavyo majani yameanza kuanguka nyuma kabisa katika mwanzo wa Agosti? Kwa nini? Ni nini kilichoyafanya hayo majani kuanguka? Ni kwa sababu kwamba u—uhai ulitoka kwenye—kwenye jani. Nao ukaenda wapi? Chini kwenye mzizi wa mti. Ni Akili gani iliyofanya uhai huo kuondoka kwenye jani na kuingia chini ardhini? Kwa sababu iwapo ungebaki hapa juu, ingeuua mti huo. Uliingia chini kwenye mzizi wa mti, kujificha, mpaka majira ya baridi kali yapite. Majira ya kuchipua yafuatayo, hurudisha uhai tena, na kuchipusha jani jingine.

39 Sasa, lazima kuwe na Akili fulani ikifanya hayo. Mti hauna akili; ni uhai tu wa mmea. Bali Akili fulani kuu huuambia mti huo, kabla ya jalidi yoyote kuupiga, kwa uhai ulioko humo ndani, "Shuka chini uingie katika mzizi wa mti, na ujifiche humo." Na basi wakati jua linapoanza kusonga nyuma, jani hilo linajuaje kwamba jua linasonga mbali na majira ya joto yanakuja? Ni Akili fulani inayoliambia hilo. Ni Mungu.

40 Ni mfano wa jinsi gani! Tunaona nini hapo? Sawa na tunavyoona katika ua; uhai, kifo, kuzikwa, kufufuka. Na hata Mungu hufanya, huyatoa maua, kwamba maua yanageuka ya kahawia, na kutengeneza shada la maua juu ya kifua cha nchi, punde tu maua yanapokufa. Jekundu, la kijani kibichi, na rangi, namna hii tu zipo hapa, alasiri ya leo.

41 Mungu si tatanishi. Watu mara nyingine wanataka kumfanya Yeye tatanishi. Bali Yeye, Mungu, anajulikana katika urahisi. Tunaangalia juu Yake, tukijaribu kumpata. Yeye ni rahisi sana, hujifanya Mwenyewe hivyo. Hiyo ndiyo humfanya Yeye kuwa mkuu sana.

42 Sasa angalia, katika huu, uhai huu uliokuwa ndani ya mti. Uliotumikia kusudi lake, ukaingia chini kaburini, kukaa mpaka wakati wa kuchipua. Sasa, Akili fulani lazima iurudishe tena, urudi na matofaa, na chochote kingine ambacho mti huo huzaa, majani yake na kadhalika. Unarudi tena.

43 Sasa, Ayubu alisema hapa, "Ee kwamba Wewe ungeniwekea muda, na kunificha kaburini, hata ghadhabu Zako zipite." Unaona kile Maandiko yalichosema? Tumefichwa kaburini mpaka ghadhabu zimepita, ndipo basi tunarudi tena.

44 "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku ya mwisho Yeye atasimama juu ya nchi; ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Aliona ufufuo ungeletwa na Mtu, siku moja; nalo swali la dhambi lingetatuliwa wakati Yule mwenye haki, Mwana wa Mungu, alikuja kufa kwa ajili ya wenye

dhambi. Hakukuwa na mtu duniani wakati huo, ama hakuna mtu tangu, aliyeweza kuunganisha njia kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mwenye dhambi. Bali Ayubu, hapa, miaka elfu nne kabla ya Kuja Kwake, aliona kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka Kwake, na kuhesabiwa haki Kwake kulikokuja kwa ufufuo, na hakikisho kamili la ufufuo wa mwaminio. Ni faraja jinsi gani kujua kwamba mambo hayo ni kweli! Si hadithi ya kubuni.

45 Tazama hapa nje. Litazame jua. Jua huchomoza asubuhi, ni mtoto mchanga amezaliwa. Mungu amelituma. Linapaswa kutumikia kusudi la Mungu. Ndipo saa tatu asubuhi, linaenda shuleni, ni tineja. Halafu basi saa sita, linakomaa kabisa. Baada ya saa sita, miaka hamsini imepita, limetumika nusu, na linaanza kuteremka, linadhoofika zaidi, kuzeeka zaidi. Linazidi kuwa na nguvu mpaka wakati huu, halafu linaanza kudhoofika.

46 Kama tu tufanyavyo. Tunaanza, tukiwa na nguvu. Na kufikia . . . Tunapofikia ukomavu wetu mkamilifu, tunakuwa na nguvu zaidi. Halafu wakati umri fulani, tuko katika ubora wetu. Ndipo tunaanza kudhoofika, wakati wote, tunashuka.

47 Hatimaye, baada ya kitambo, linatua kwenye upeo wa magharibi, nuru ya kupendeza. Lilitumikia kusudi la Mungu. Linakufa. Nchi inaingia baridi, inatulia, inakuwa baridi, usiku kucha. Sasa je! huo ndio mwisho wa hilo jua? Je! hiyo ndiyo mara ya mwisho utakayopata kuliona? La. Asubuhi inayofuata, huchomoza tena, katika ufufuo. Mungu, kila siku, akilishuhudia, kasema, "Kuna uhai, kifo, kuzikwa, kufufuka."

48 Kila kitu unachoangalia hunena vivyo hivyo, "uhai, kifo, kuzikwa, na kufufuka," hiyo ni, kikitumikia kusudi Lake.

49 Sasa kunaweza kuwa na wakati ambapo ua hili lingeweza kuwa ua na lisingeweza kuishi tena. Hiyo hapo hoja ambayo ningependa, na iwapo Garnett angeweza kuzungumza nami, alasiri ya leo, hili hapa jambo ambalo angetaka niseme, maana yeye yuko katika Uwepo wa Mungu. Ikiwa mbegu hiyo . . .

50 Wengi wenu enyi wanaume hapa alasiri ya leo ni wakulima, ama mnaishi karibu hapa ambapo mnaona ma—mashamba na kuona maumbile. Mbegu ikipandwa, haijalishi jinsi mbegu hiyo inavyoonekana ya kupendeza, kama mbegu hiyo haijarutubishwa, haitaishi. Itaingia ardhini, na itaoza, na huo ndio mwisho wake. Hamna njia, hata kidogo. Hakuna kitu mle kurudi kuwa hai. Mbegu hiyo haina budi kuwa katika chavua pamoja na mwenzi wake la sivyo haitafufuka tena.

51 Na hicho hapo kile kinachofanya hakikisho letu la kufufuka tena. Kama Yesu alivyotwambia, "Mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuona Ufalme wa Mungu." Tumewekwa hapa ili kufanya chaguo.

52 Na sasa ua hilo la kupendeza . . . haijalishi jinsi lilivyo la kupendeza, na jinsi mbegu ilivyo nzuri na duara. Kama

vile mhindi chotara, tungeweza kupanda mhindi chotara, hautafanya chochote. Ni mbegu nzuri, isiyo na uhai. Uhai wake umepotoshwa.

53 Na uhai wowote uliopotoshwa kutoka kwa Mungu hauwezi kuishi tena. Lazima tuzaliwe tena.

54 Lakini kwa hakika kama vile mbegu hiyo imerutubishwa, ni hapo ndipo inafufuka tena. Hakuna njia ya kuizuia isifufuke tena. Haina budi kufufuka, kwa sababu imerutubishwa na uhai wake wa mmea umo ndani yake.

55 Sasa, mwaminio anao Uhai wa Kristo ndani yake, Yule aliyefufuka kwanza kwa ajili ya kutuhesabia haki, kuthibitisha kuna ufufuo wa uhai wa mwanadamu, mwili wa mwanadamu, kwamba tunaishi tena kwa kuwa tumerutubishwa; kwa maneno mengine, kuzaliwa tena, na Roho Mtakatifu.

56 Na kila kitu ambacho tungeweza kuona katika maumbile . . . ninasimama hapa na ninayo mambo mengi niliyoandika kwenye kijipande cha karatasi hapa, ambayo ningependa kuwazungumzieni kuyahusu. Lakini hayo yanafaa kutosheleza, kuwafanya mjue kwamba huwezi kutazama nje pasipo kuona ushahidi wa kifo, kuzikwa, na kufufuka. Popote uendapo, chochote unachoangalia, haiwezekani kupita juu ya: kifo, kuzikwa, kufufuka.

57 Halafu basi, tena, tunaona kwamba ufufuo huja tu kama unatumikia kusudi la Mungu. Kama hautumikii kusudi la Mungu, haijalishi jinsi ilivyo ya kupendeza, jinsi—jinsi inavyoonekana maridadi, na jinsi ambavyo huenda ikaonekana bora kuliko Mbegu nyingine iliyorutubishwa, haitafufuka kamwe. Inaishi haya, na hiyo yatosha. Lakini kama Hiyo imerutubishwa, lazima ifufuke tena.

58 Ndivyo ilivyo, rafiki zangu, sisi hapa alasiri ya leo, kuona kile ambacho kifo kimemfanyia ndugu yetu. Haina budi kurutubishwa. Huenda tukawa washiriki wa kanisa. Huenda tukawa watu wema. Huenda tukawa m—mtu mzuri katika ujirani; baba mzuri, mama, mwana, binti. Lakini isipokuwa tumerutubishwa na Roho wa Mungu, hatutafufuka katika ufufuo. Imekwisha.

59 Inatuzungumzia kuhusu mambo haya. Maumbile huita, siku baada ya siku. Nalo jua huchomoza na kutua. Mwezi na nyota hutokea, jambo lile lile. Kila kitu katika maumbile huzunguka katika kitu kimoja: kifo, kuzikwa, kufufuka; kifo, kuzikwa, kufufuka. Kila siku ya maisha yetu, kitu fulani kinashuhudia kwetu: kifo, kuzikwa, kufufuka.

60 Tunatembea juu yake, mara nyingi. Hebu tusifanye hivyo. Hiyo siyo sababu yake kuwekwa hapa, na ulimwengu kuwekwa katika utaratibu namna hiyo. Ni kwa ajili ya Uzima wa Milele, tunaojua. Na kuona juu ya mbegu hizi, kwamba hazijarutubishwa na kutumikia kusudi la Mungu, haiwezi

kufufuka. Wala nasi hatutafufuka, ingawa sisi ni watu wema, ingawa sisi ni washiriki wa kanisa, ingawa sisi ni majirani hodari, watu wazuri, walioelimika, werevu. Sayansi inaeleza kile ambacho kimekuwako. Sayansi haiwezi kutoa uhai.

61 Uhai ni wa Mungu, pekee, na Yeye pekee Ndiye hushughulikia uhai. Kwa hiyo hatuna budi kufikia mahali hapo, kurutubishwa na Neno la Mungu, la sivyo hatutafufuka tena. Uhai we—we—wetu unaisha kabisa wakati—wakati tunapomaliza maisha haya hapa, hiyo hufanya hivyo, kabisa, ikiwa sisi—ikiwa sisi hatujarutubishwa na—na Neno la Mungu, au na Uzima wa Mungu.

62 Sasa, maskini, mwili huu baridi uliolala hapa, hakuna mmoja wetu awezaye kusema ila kwamba ni sehemu ya uchumi huu mkubwa wa maumbile ya Mungu. Yeye ni sehemu ya maumbile ya Mungu. Yeye ni mtu, mwanadamu ambaye Mungu aliumba. Amelala, usingizi sasa. Sasa, jambo ni kwamba, ikiwa alitumikia kusudi la Mungu katika maisha yake, basi lazima kuwe na kufufuka kwa Garnett. Hakuna njia ya kukwepa huo. Huu si mwisho wa Garnett.

63 Vema, sisi sote hatuna budi kuchukua njia hii kupitia uhai. Tunakuja kutoka kwenye giza na kuingia njia iyo hiyo. Na kila mmoja wetu, njia moja ama nyingine, tunapitia kwenye kivuli, bonde la vivuli vya mauti. Lakini kitu ambacho kilifanya tuwekwe hapa, kuna . . .

64 Kama vile ulimwengu. Yesu alisema, “Huwezi kutumikia Mungu na mali.” *Mali* ni “ulimwengu.” Huwezi kumtumikia Mungu na ulimwengu kwa wakati mmoja.

65 Tuna chaguo letu. Tunaweza kurutubishwa na Mungu, kwa Roho Wake Mtakatifu, na tuwe na Uzima wa Milele. Tusipofanya hivyo, tukifa, huo ndio mwisho. Tuko tayari kwa Hukumu basi, ni kwa nini hatukufanya hivyo, halafu adhabu. Inafuata hiyo, kwa kukataa Hilo.

66 Lakini, nina furaha sana, kadiri nijuavyo, niwezavyo kufahamu, kwa Neno la Mungu na kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu, mvulana huyu alitimiza hali hiyo. Alizaliwa kwa Roho wa Mungu, mtu aliyebadilika. Roho wa Mungu alikuwa juu ya jamaa huyo mdogo. Alikuwa Mkristo mwaminifu. Alitumikia kusudi la Mungu. Labda ilikuwa ni kwa muda mfupi.

67 Lakini Mungu wakati mwingine huwafunza watu kwa miaka, ili kupata huduma ya siku chache kutoka kwake. Yohana Mbatizaji alikuwa miaka thelathini, peke yake, nyikani, kwa ajili ya huduma ya miezi sita. Yesu Kristo alikuwa na umri wa miaka thelathini, kwa ajili ya huduma ya miaka mitatu, kwa ajili ya kusulubiwa. Mungu huwafunza watu, huwakuza. Ni kusudi Lake. Wakati uko na mwanadamu. Umilele uko na Mungu.

68 Ninaamini kwamba Mungu alimleta mvulana huyu mdogo hapa duniani kwa kusudi.

69 Basi kama ulitambua, moja kwa moja kwenye wakati wa u—ugonjwa wake na kadhalika, huu ulimshika kwa kusudi fulani. Mungu angaliweza kumfanya mvulana huyo mzima na mwenye afya. Lakini Yeye alifanya nini badala ya kuchukua uhai wake? Alimwacha ainuke mahali tu ambapo hakuwa anaenda kufa.

70 Na wala ugonjwa wa kupooza haukumwua. Hakufa kwa ugonjwa wa kupooza. Hakuna ugonjwa mwingine uliomwua, ambao tuliombea, mimi na yeye, na Wakristo wengine hapa karibu Campbellsville, waliomwombea. Kamwe haukumwua. Huo haukumwua. Mnaona?

71 Ulikuwa ni wakati wa Garnett kuondoka. Lazima aondoke. Alikuwa ametumikia kusudi lake. Alimjia Kristo, amerutubishwa. Vipi kama angalikufa kabla ya wakati huu? Ugonjwa wa kupooza ulimpeleka kwa Mungu. Alikuwa awe dalali wa tumbaku, kile alichokuwa nacho niani. Hilo halikuwa kusudi lake, hata kidogo. Tulijua hilo. Kusudi lake lilikuwa ni kuwa Mkristo.

72 Sasa, dalali wa tumbaku, mtu fulani alisema, labda miaka sabini na mitano kuanzia leo, kama ulimwengu utasimama muda huo, "Garnett, yeye alikuwa ni dalali mashuhuri." Labda hayo ndiyo yote mhudumu angeweza kusema kwenye mazishi yake, "Alikuwa ni dalali mashuhuri."

73 Lakini tunaweza kusema nini leo? "Yeye ni Mkristo." Kama dalali, bila chembe ya Uzima, kumbukumbu tu la kizazi hicho, angekuwa ameenda, miongoni—miongoni mwa watu wachache. Sasa yuko miongoni mwa wasiopatikana na mauti. Hana budi kuja katika ufufuo. Hakuna njia ya kumwepusha na huo. Hana budi kuja, kwa kuwa alitumikia kusudi lake. Alirutubishwa na Roho Mtakatifu wa Mungu, wa Uzima wa Milele uliokuwa ndani ya mvulana huyo. Kwa wingi sana, ambapo kama angesema, "Kama ningejua . . . "

74 Mara ya mwisho nilipozungumza na yeye, alisema, "Kama ningalijua kuwa nilikuwa na . . . ningeweza kuwa mzima, mwenye nguvu kama wavulana hawa wengine, nikikimbia huku na huko hapa barabarani nikiwa na gari langu lenye mbio kuzidi magari yote, nikikimbia huku na huko barabarani, na kunywa pombe, na nisingejua Hiki ambacho ninajua," alisema, "Nisingelibadilisha Hiki kwa ajili ya maisha elfu kumi namna hiyo." Mvulana mdogo wa umri wa miaka kumi na minane, kijana mwanamume mzuri anayeonekana wa kupendeza, labda angekuwa lengo la kawaida kwa ibilisi.

75 Lakini ilibidi Mungu amtupe ndani kwenye umri huo, ili kupata kutoka kwake, kutumikia kusudi. Angalia subira yake, shuhuda zake miongoni mwenu majirani. Angalia kile alichokuwa, kile, jinsi maskini maisha yake yalivyonenea wengi wenu, kwamba kwenye Siku ya Hukumu, bila ya hicho, maisha

yake yatashuhudia moja kwa moja dhidi yako. Alikuwa ni mfano wa kile Mungu alichotaka naye. Alitumikia kusudi la Mungu.

76 Sasa, kama alitumikia kusudi la Mungu na amerutubishwa, kama vile maumbile yote hayana budi kurutubishwa, pamoja na ahadi kwamba atafufuka tena, tungewezaje kutilia shaka ufufuo, wa kumwona Garnett tena? Mbona, ingekuwa kabisa ni wendawazimu kusema kwamba hawezi kufufuka. Garnett asipofufuka, kamwe hakujawahi kuwa na jua lililochomoza na kutua, na kuchomoza tena. Garnett asipofufuka, ua kamwe halifi na kuishi tena. Lilitimiza kusudi la Mungu. Lilitumikia kusudi la Mungu. Lilirutubishwa na uhai, nalo likachipuka tena. Vema, sisi—sisi tungekuwa ki—ki—kitu cha kuchukiza, kitu cha kijinga, kusema hakuna ufufuo, wakati tukiangalia moja kwa moja nje, ndani, na kuona ku—kusudi la ufufuo na kile kitupasacho kuwa ili kuwa na ufufuo.

77 Garnett ataishi tena. Yu hai sasa. Yuko katika ulimwengu mwingine. Naye atafufuka tena kwa hakika tu kama vile ua hufufuka tena. Atafufuka tu kwa hakika—hakika kama vile mwezi, jua au nyota hufufuka tena. Atafufuka. Lakini, unaona, hizo hufufuka tu kwa maisha mengine yapatikanayo na mauti, kutoa ushuhuda kwa kipindi kingine. Wakati akifufuka, itakuwa mwishoni mwa wakati, hakutakuwa na ushuhuda tena. Yeye anao Uzima wa Milele. Hilo lilikuwa na maisha ya kuendelea; halina budi kurutubishwa kwa ajili ya—kwa ajili ya maisha ya kuendelea, kulifanya lifufuke tena kwa ajili ya—kwa ajili ya maisha ya kuendelea. Yeye amerutubishwa na Uzima wa Milele. Basi wakati akifufuka tena, hakuna tena mauti, anaishi milele.

78 Nimehubiri maelfu ya matanga katika siku zangu, kote ulimwenguni. Laiti ningaliweza kusema, juu ya matanga hayo mengi ambayo nimehubiri, ningeweza . . . Laiti ningaliweza kusema maneno ambayo ningeweza kusema juu ya Garnett, na matumaini niliyo nayo kwa Garnett. Na nikijua kwamba Mungu atamfufua, kwa sababu alitimiza kila hitaji nijualo, ambalo Mungu alihitaji. Nayo maisha yake yalionyesha ua la Roho Mtakatifu lilikuwa ndani yake, kwamba Mungu aliishi ndani yake. Mvulana huyo alikuwa ni mvulana aliyebadilika. Hapana shaka hata kidogo. Maisha yake yalishuhudia jambo hilo. Alibadilishwa.

79 Sasa, kama tungaliweza kusema kwamba, "Hakuna ufufuo tena, na huu ndio mwisho wa Garnett. Garnett, yote tutakayoona ni wakati tutamzika huko nje, alasiri ya leo." Basi ni kitu gani kinachomzungumzia? Kama mtu fulani angesema, "Loo, sijui kuhusu hilo. Sijui. Sasa, si—sijaona hilo likifanywa." Hakika, mwisho wa wakati haujawadia bado. Lakini unaposema hivyo, jambo la kwanza litakalokubidi kufanya . . .

80 Neno la Mungu linamshuhudia Garnett. Neno la Mungu lilisema, "Sisi tulio hai na tuliosalia hata Kuja kwa Bwana

hatutawazuia au kuwachelewesha wale waliokwisha kulala mauti. Maana parapanda ya Mungu italia, nao waliolala katika Kristo watafufuka kwanza; nasi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, kumlaki Bwana hewani." "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi." Maandiko! "Mimi ndimi ufufuo na Uzima," asema Mungu. Unaona? Ingekubidi kushuhudia dhidi ya Neno la Mungu. Neno la Mungu linamshuhudia mvulana huyu. Basi ni kitu gani kinachotosheleza zaidi ya Neno la Mungu Mwenyewe? Ambalo, Yeye ni Neno Lake. Neno ni Mungu. Naye Mungu, Mwenyewe, anashuhudia kwamba Garnett atafufuka. Garnett atafufuka tena.

81 Maumbile yote! Ingetubidi kusema, "Jua halichomozi. La, Mungu alikosea. Jua, hatulioni jua." Unaona? Lingekuwa ni jambo la kiwendawazimu.

82 Jua linasema kuwa atafufuka tena. Ua linasema atafufuka tena. Neno linasema yeye atafufuka tena. Kila maumbile, maumbile yote, yanasema kwamba atafufuka tena. Dunia, ikigeuka, inasema yeye atafufuka tena, kila kitu ambacho unakiona. Hata kwa Neno la Mungu! Ninii pekee...Roho Mtakatifu, ndani ya kifua changu na Wakristo wengine waaminio hapa, anadunda sasa kwa imani, inayosema yeye atafufuka tena.

Basi utaruka juu ya imani yako, uruke juu ya Neno la Mungu, uruke juu ya maumbile, uruke juu ya kila kitu, unaona, ukisema hatafufuka.

83 Huu sio mwisho wa Garnett. Huu ni mwisho wa kusudi lake juu ya maisha du—duniani, lakini atafufuka tena. Unaona? Kitu chote: atafufuka tena. Kwa hiyo sisi ni nini, mahangaiko yetu ni nini?

84 Bila shaka, tunachukia kumwona huyo jamaa mdogo amelala hapo namna hiyo, inaonekana kama ni katika ubora wa maisha. Lakini unajua wakati Mungu...Ukichuma ua kutoka kwenye shamba lako la maua, huchukui yaliyozeeka kila mara. Wakati mwingine inakubidi kuchukua chipukizi, chipukizi inabidi litumikie kusudi lako katika shada la maua. Labda Mungu alitaka chipukizi. Na hicho ndicho Yeye alikichukua hapa, kwa ajili ya chipukizi kwa Madhabahu Yake Utukufuni; pamoja na hakikisho, la kila kitu kikishuhudia kwamba atafufuka tena. Imani yetu inasema anafufuka tena. Neno linasema anafufuka tena. Mwezi unasema anafufuka tena. Nyota zinasema atafufuka tena. Jua, maua, maumbile, kila kitu kinasema anafufuka tena.

85 Kwa sababu, wote waliomjua Garnett, walijua hili, kwamba alikuwa Mkristo. Usingeweza kuja katika uwepo wake pasipo kujua kulikuwa na badiliko ndani ya mvulana huyo. Alikuwa amerutubishwa na Uzima.

86 Ombi langu ni kwamba sisi tulio hai, alasiri ya leo, tutaona mfano wa kile—wa kile Mungu afanyacho, na tutajiandaa. Na tusipojiandaa, hatuna chembe hii ya Uzima wa Milele, tukijua kwamba lazima tuende njia iyo hiyo anayoenda, hebu na turutubishwe. Hebu tumpokee Kristo ndani ya mioyo yetu na tuzaliwe tena. Kwa sababu, ndugu, dada, kila mmoja wetu anakabiliana na hili, haijalishi wewe ni nani, ni kiasi gani cha biashara uliyo nayo, jinsi ulivyo kijana au mzee, inakubidi kukutana nalo. Inakubidi kukutana nalo. Pia usi—usithubutu kujaribu kufanya hivyo bila kwanza kurutubishwa na Kristo, kwamba unao Uzima wa Milele.

87 Ndipo, kifo kimemezwa katika ushindi. Garnett atafufuka tena. Maumbile yote. . . Sasa, katika ujirani, kila mtu alimfahamu mvulana huyo. Kila mtu aliyewahi kukutana naye anajua yeye alikuwa ni Mkristo. Sasa, Neno la Mungu na maumbile yote yanasema yeye atafufuka tena.

88 Mama yake, baba yake, jamaa zake wote, chochote kile, enyi watu hapa mnaomtazama; kama mhudumu wa Injili, kama ndugu yake, sioni chochote katika Neno la Mungu wala chochote katika maumbile. . .

89 Sababu ya mimi kuchagua kusema hili, labda mtu fulani hataenda kanisani sana na kuelewa hilo. Niliwazia, katika njia hii, ingefanya kila mtu kuelewa. Njia ndogo tu rahisi unayoangalia hapa nje katika maumbile na kuona kile—kile kilichofanyika.

90 Garnett alitimiza kipimo kamili cha Mungu. Alitumikia kusudi la Mungu. Yeye hajafa. Yu hai milele, akingojea tu wakati fulani kwa ajili yetu kuja.

91 Sasa, nyinyi mliokuwa na Garnett maishani, baba yake, mama, kaka, dada, na chochote ulichokuwa, jamaa, mlimjua. Mlimpenda. Usingeweza kukutana na Garnett bila ya kumpenda. Unaona? Mlikuwa na yeye hapa. Sasa vipi kuhusu maisha ya baadaye? Hebu tujitayarishe, kwamba sisi pia tutakutana naye katika ufufuo. Hebu tuyaweke maisha yetu katika njia, hata tutakutana na yeye katika ufufuo.

92 "Mtu akifa," lilisema andiko, "anaweza kuishi tena? Siku zote nilizowekewa za maisha yangu nitangojea, hata badiliko langu lije. Wewe utaita, nami nitajibu." "Parapanda ya Mungu italia, nao waliolala mauti katika Kristo watafufuka kwanza. Ndipo tukiwa hai kwenye wakati huo na tumesalia, tutanyakuliwa pamoja nao, kukutana na Bwana hewani, na kuwa na Bwana milele."

93 Huu ni uwanja wa kuthibitishwa, wakati wa kujaribiwa. Garnett alitimiza vipimo kamili ambavyo Mungu alihitaji. Basi leo, Garnett hajafa, analala pamoja na Yule ambaye anampenda zaidi ya chochote kingine ulimwenguni. Zaidi ya alivyopenda. . . Kadiri vile alivyowapenda wazazi wake, alimpenda kila mtu

aliyekutana naye, alipenda. Hata hivyo, Yule aliyempenda upeo alikuwa Yesu Kristo. Ameenda kuwa pamoja na Yeye. Na nyinyi mlioshiriki upendo wake mdogo, hebu sote tujitayarishe kukutana na yeye kwenye ule ufufuo mkuu.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

94 Huku tumeinamisha vichwa vyetu. Sijajaribu kusema mengi sana juu ya Garnett. Yeye ni Mkristo. Maisha yake mwenyewe hueleza kile alicho. Lakini jambo nililojaribu kuwaambieni, enyi wapendwa, kwamba atafufuka tena. Kuwathibitishieni, huu si mwisho. Kuna hakikisho lililoandikwa, na Damu ya Mwana wa Mungu, yeye atafufuka tena.

95 Sasa hebu tuandae mioyo yetu sasa, ili wakati sisi pia tutakapoletwa mahali kama hapa, ukumbi fulani wa mazishi, kwamba wapendwa wetu waweze kukumbuka kwamba sisi pia tumejitayarisha kwenda. Na hebu baba, mama, wapendwa wa mvulana huyu mdogo, jambo kuu zaidi . . .

96 Mnajua, ninajua jinsi mnavyoteseka. Ndiyo kwanza nimwachilie mtoto, msichana mdogo. Ninajua jinsi mioyo yenu ilivyojaa huruma.

97 Lakini, mnaona, kama Garnett angalikuwa amepotea, ungekuwa ni wakati wa kutisha mno kwenu. Bali ni saa yenye utukufu jinsi gani kwenu, kujua kwamba mvulana wenu alikuwa pamoja na Kristo. Na ilimbidi kuondoka wakati fulani. Na katika mwisho wa safari, angali alidumu na imani yake. Basi Mungu anaye leo. Kwenu nyinyi ambao ni mabinamu na jamaa zake, wazieni tu kile alichokuwa. Na sasa vipi kama angalikuwa ameenda njia nyingine? Hatuna chochote cha kufadhaikia. Garnett yuko pamoja na Yesu. Hebu na tujitayarishe kwenda pamoja na Yeye, pia.

98 Mungu mwenye neema, Yehova mkuu wa Milele, Yule aliyetembea juu ya maji na kusema, "Iwe nuru." Wewe Ambaye ulinena ulimwengu ukawepo kwa Neno Lako, umeahidi kwa Neno lilo hilo kwamba tutafufuka tena. Sasa tunataka kukutolea, Wewe, Baba, alasiri ya leo . . .

99 Kama nilivyoshirikiana na huyu ndugu kijana, maishani, na jinsi upendo usiokufa kati yangu na yeye. Mradi ninaishi hapa, nadhani daima nitamkumbuka huyo askari hodari wa vita akisumbuka kwenye kitanda kile, katika mashine ya kuvutia hewa, kati ya pumzi, akimsifu Bwana Mungu. Alikuwa mfano, pia, kwangu mimi, wa subira yake, asilalamike kamwe, ila tu, "Ma—mapenzi ya Mungu yafanyike." Wewe umemweka mbele zetu, na sasa Wewe umemwondoa katika uwepo wetu.

100 Bwana Mungu, jalia kila mmoja wetu, alasiri ya leo, tulio hai . . . Pia ninajihisi, labda, kwamba Garnett angenitaka niseme hili. Ikiwa hatuko tayari, jalia tujitayarishe, na tuwe kama nilivyosema, Baba, waliorutubishwa, kukutana na yeye kwa

Roho Mtakatifu yule yule ambaye alimpokea, Uzima uliokuwa ndani ya Kristo.

101 Mbariki huyu mama mpendwa na huyu baba, na wazazi, na wapendwa. Yeyote yule waliye, jalia Uwepo Wako mtakatifu uwe pamoja nao, Baba. Naomba huu uwe wakati ambao—ambao watawaza, zaidi ya walivyowahi, kile kilichofanya maisha haya madogo kuishi namna hii. Yalikuwa ni ushuhuda, kama mfano.

102 Kwa vijana wanaume wanaoketi hapa, ambao walishirikiana naye, kama mvulana mdogo, wakaona kile alichokuwa hapo kabla, na kisha kile alichokuwa baadaye. Hebu maisha yake yawe ma—mahubiri kwao, Baba, kwamba, pia, kwamba waweze kujiandaa kukutana na maskini rafiki yao upande ule mwingine, ambapo hapatakuwa na mauti tena, au huzuni, hakuna tena huzuni kubwa. Tujalie, Bwana.

103 Nasi watu wazee, ambao walimwona kijana huyu mwanamume, moja kwa moja katika ubora wa maisha, na kumwona akibadilika, na kuja kutoka kwenye maisha ya kufa hadi kwenye maisha ya Uzima. Tujalie, Bwana, kwamba tuweze kuona hilo, alasiri ya leo, kwa urahisi wa kutumia mifano ya maumbile, kisha kuiweka tena kwenye Neno la Mungu, kwenye ahadi. Na Wewe ulisema, "Neno la Mungu ni mbegu." Nayo mbegu lazima izae ya jinsi yake.

104 Ninaomba ya kwamba Wewe utawabariki na kuwafariji watu hawa. Wajalie kujua kwamba maskini mvulana huyu aliwekwa tu hapa kwa ajili ya mahubiri. Amekwishahubiri mahubiri yake, Kitabu kimefungwa, bali tutamwona tena. Jalia, Bwana, kwamba sisi sote tutasimama huko katika uzuri wa Kristo, ambapo tuna Uzima wa Milele. Hadi wakati huo, tudumishe tumewekwa katikati ya mapenzi Yako. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

MIMI NDIMI UFUFUO NA UZIMA SWA63-1118
(I Am The Resurrection And Life)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu alasiri, tarehe 18 Novemba, 1963, kwa ajili ya mazishi ya Ndugu Garnett Peake katika Nyumba ya kutayarishia Mazishi ya Lyon kule Campbellsville, Kentucky, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org